SAYYID AHMAD BIN HAMID MANSAB AAL SHEIKH ABUBAKAR BIN SALIM

(1928 AD – 1977 AD)

SAYYID AHMAD BIN HAMID MANSAB IBNI SHEIKH ABUBAKAR BIN SALIM

Jina lake

Sayyid Ahmad bin Hamid bin Ahmad (Mansab) bin Ali Itibari bin Mwinyi Mkuu Sultan Ahmad bin Ali Al-Huseyniy, nasabu yake imefika kwa Sheikh Abubakar bin Salim na kupitia kwa Habib Abdulrahman Saggaf na kuungana kwa Imam Faqihul Muqaddam hadi kufika kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

Wazee wake

Sayyid Ahmad Hamid ametokana na wazee watukufu, baba yake Sayyid Hamid Mansab alikuwa mwanachuoni mkubwa wa kupigiwa mfano.

Kuzaliwa na kulelewa kwake

Amezaliwa mwaka 1928 AD sawa na mwaka 1346 AH takriban katika mji wa Zanzibar Afrika Mashariki.

Alilelewa na wazazi wake wawili na kupata malezi mazuri pamoja na kusomeshwa masomo ya Sekula na ya dini kwa walimu mbalimbali.

Kusoma kwake hadi kwenda Tareem Hadhramout

Sayyid Ahmad bin Hamid alibahatika kupata msingi wa masomo ya dini kutoka kwa wanavyuoni tofauti waliokuwepo zama hizo. Alisoma kwa baba yake mzazi ambae alikuwa miongoni mwa wanachuoni wakubwa pamoja na kusoma Ukutani na kwa mashekhe wengine. Pia alipata msingi mzuri wa masomo ya

Sekula na kumaliza ("0" Level) katika skuli za Serikali (Government school) na kufaulu mitihani ya Cambridge, kwa wakati huo ilikuwa ni daraja kubwa mtu kuifikia.

Baada ya kumaliza masomo ya skuli alitaka kujiunga Makerere chuo kikuu cha Uganda na hadi kukubaliwa lakini baba yake akaamuwa kumpeleka Hadhramout akasome zaidi masomo ya dini.

Sayyid Ahmad Hamid alijiunga Ribat ya Tareem akiwa na umri wa miaka 22 takriban. Alifika Tareem katika mwezi wa Shaaban mwaka 1368 AH na kuanza masomo yake na kudumu kwa kipindi cha miaka kumi (10) bila ya kurudi kwao.

Alipokuwa Ribat alisoma kwa mashekhe wengi sana kuanzia kwa vijana hadi kwa watu wazima, kutokana na uhodari wake alifikia kusoma mpaka vitabu vikubwa kwa mashekhe wakubwa akishirikiana na maustadhi wake.

Sayyid Ahmad Hamid alirudi kwao Zanzibar mnamo mwezi wa Rajab mwaka 1378 AH sawa na mwaka 1959 AD takriban akiwa amejaa elimu katika Fati tofauti.

Miongoni mwa mashekhe zake wa Zanzibar:

1. Habib Omar bin Ahmad bin Sumeit.
2. Sayyid Hamid bin Mansab ibn Sheikh Abubakar bin Salim.
3. Sheikh Suleyman bin Muhammad Al-Alawy.
4. Sheikh Abubakar bin Abdallah Bakathir.
5. Sayyid Ahmad bin Husein ibn Sheikh Abubakar bin Salim.
6. Sayyid Alwy bin Abdul-Wahab Jamalu-leyl.

Baadhi ya mashekhe zake wa Hadhramout:

1. Habib Alwy bin Shihab.
2. Habib Abubakar bin Muhammad Sirriy.
3. Habib Muhammad bin Salim bin Hafiidh.
4. Sheikh Salim bin Said Bukeyyir.
5. Sayyid Hassan bin Abdallah Shatry (wakati huo akiwa kijana).
6. Sayyid Abdul-qadir bin Abdulrahman Al-Juneyd (baadae wakawa wanasoma pamoja kwa mashekhe wakubwa).

Kazi alizofanya na kusomesha kwake

Sayyid Ahmad Hamid aliporudi kutoka masomoni Hadhramout alianza kusomesha chuo cha Muslim Academy (Maahad Islamiy ya Zanzibar) iliyokuwepo Forodhani mjini Unguja, wakati huo Maahad Islamiy iliongozwa na Mudir wake Sayyid Omar Abdallah (Mwenye Baraka).

Aliendelea kusomesha hapo hadi Maahad ilipofungwa mnamo mwaka 1964 AD akasomesha skuli ya Vikokotoni (Arabic speaking) na baadae alisomesha skuli ya Kidutani (Taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni).

Kilipofunguliwa chuo cha Kiislamu cha Mazizini mwaka 1972 AD, Sayyid Ahmad Hamid alikuwa ni miongoni mwa walimu wa mwanzo bali pia alikuwa katika safu ya Uongozi. Mwalimu mkuu wakati huo alikuwa Sheikh Mussa Makungu na yeye Sayyid Ahmad Hamid akawa naibu wake na aliendelea na kazi hiyo hadi kufariki kwake.

Ama kwa upande wa darasa za misikitini Sayyid Ahmad bin Hamid alikuwa na darsa nyingi, takriban alisomesha kila siku baina

ya Maghribi na Isha katika Msikiti wa Ijumaa wa Forodhani msikiti ambao alikuwa akidarasisha baba yake Sayyid Hamid Mansab. Pia alikuwa anasalisha na kutoa khutba za Ijumaa hapohapo msikiti wa Ijumaa wa Forodhani.

Kwa upande wa darasa za mwezi wa Ramadhani alikuwa akisomesha msikiti Gofu baada ya kufariki baba yake.

Sheikh Suleyman Al-alawy wakati yupo Dar es Salaam anauguwa alimtaka Sayyid Hamid Mansab adarasishe Ramadhani Msikiti Gofu na pindi akidharurika adarasishe mwanawe Sayyid Ahmad bin Hamid. Sayyid Hamid Mansab alipoanza darsa hiyo siku ya Ijumaa Ramadhani mosi ya mwaka 1385 AH sawa na tarehe 25/12/1965 akafariki dunia hapo hapo msikitini wakati wa Laasiri akiwa darasani, na baada ya mazishi akashika darasa mwanawe Sayyid Ahmad bin Hamid.

Sheikh Suleyman Al-Alawy aliporudi katika matibabu yake aliendelea na darasa za Ramadhani mpaka kufariki kwake mwaka 1970 AD na baadae akaendeleza Sayyid Ahmad bin Hamid Mansab hadi kuaga kwake dunia.

Wanafunzi wake

Sayyid Ahmad Hamid aliwasomesha watu wengi sana wa kila namna nayo inatokana na kusomesha sehemu nyingi katika uhai wake. Wapo wanafunzi wa Muslim Academy, chuo cha Kiislamu, Skuli, darsa za Msikitini, aidha baadhi ya waliokuwa wakidumu kwenye darsa zake ni pamoja na wale aliosoma nao Sekondari kama Hajji Yusuf Mshangama na Bwana Ahmed Abubakar Bwamzee na wengineo.

Wengi wa vijana waliobahatika kusomeshwa na bwana huyu wapo hai katika zama tulizonazo, kila mmoja ameinukia na fani yake kulingana na umahiri alionao, bali wengine ni wafanyabiashara, walimu, watendaji maofisini nakadhalika.

Wapo wengine wameinukia kuwa ni Mashekhe na wengine ni viongozi wanaotegemewa.

Miongini mwa wanafunzi wake:

1. Sheikh Bwanakheir Hassan.
2. Bwana Said Ilyas.
3. Maalim Abdalla Bakathir.
4. Sheikh Mohammad Mlamali.
5. Bwana Abdul-Hamid (wa Agriculture).
6. Bwana Kassim Zaharani.
7. Sheikh Imamu (aliyekuwa akilelewa nyumbani).
8. Sayyid Harub bin Abdallah Al-Busaid.
9. Bwana Ahmad Muhammad Abubakar (Sungura).
10. Sayyid Ahmad Abadalla Shatry.
11. Sheikh Ali Hemed Jabir (Maalim Aliyan).
12. Sayyid Shihab bin Hassan Sheikh.
13. Sheikh Khamis Abdulhamid.
14. Sayyid Muhammad Abbas Jamaluleyl.
15. Sheikh Ahmad Himid Mbaye.

Na wengi wengineo.

Tarika yake na Madhehebu yake

Sayyid Ahmad bin Hamid alikuwa na Aqida ya Ahli-Sunna Waljamaah, akifuata Madhehebu ya Imam Shafii na Tariqa yake ni ile ya babu zake ya Aal Baalawy.

Hadhi yake

Sayyid Ahmad Hamid aliporudi masomoni nchini Hadhramout alianza kusomesha akishirikiana na baadhi ya mashekhe zake, lakini haikupita miaka mingi mashekhe zake wengi walifariki hivyo ikawa yeye ndie anaerejewa kielimu na kutangulizwa katika Majlisi za kheri pamoja na kuwa na umri mdogo.

Sifa zake

Sayyid Ahmad bin Hamid aikuwa na sifa nyingi nzuri ambazo zilipelekea kukubaliwa na watu wa kheri, alisifika na ujasiri, upole, usikivu, usaidivu, mwenye hikma, akiwapenda wanafunzi, fasaha anapodarasisha au anapotoa mawaidha, mwenye unyenyekevu (Tawadhui), mwenye adabu nyingi kwa mashekhe zake.

Sayyid Ahmad Hamid alikuwa anajuwa Kiingereza vizuri hadi baadhi ya matajiri walimuomba awasomeshe watoto wao Kiingereza alipokuwa Tareem na watampa ujira mkubwa wa fedha lakini alikataa kwa lengo la kuchunga heshima ya mashekhe waliomtangulia na heshima ya mji wa Tareem. na sifa nyenginezo.

Kufariki kwake

Sayyid Ahmad Hamid alifariki siku ya Jumapili tarehe 21 Rabiul Aakhar 1397 AH sawa na tarehe 10/4/1977 AD akiwa na miaka 52 takriban na kuzikwa pembeni mwa alipozikwa baba yake katika kiunga cha Makaburi yaliyopo Ukutani mjini Unguja.

Familia yake

Sayyid Ahmad bin Hamid alipofariki aliwacha kizuka mmoja Bi Amina bint Sayyid Ali Al-Maarouf (Bi Koko), bibi huyu alikuwa ni mja wa kheri na alipata malezi kutoka kwa Habib Omar bin Sumeit.

Sayyid Ahmad bin Hamid hakujaaliwa kupata mtoto hadi kufariki kwake. Pia aliwaacha ndugu zake kwa baba mmoja ambao watatu wanaume Sayyid Muhammad, Sayyid Saleh na Sayyid Husein na ndugu wawili wakike.

Rejea:

1. *Kitabu "Baadhi ya Wanavyuoni wa Afrika ya Mashariki" Sheikh Abdalla Saleh Farsi.*
2. *Kitabu "Uqudul-Jaahizah" Sayyid Abdulqadir Al-Juneyd.*
3. *Baadhi ya wanafamilia na wanafunzi wake.*

Maahad Juneyd Islamiy

Kitengo cha Bahthi na Utafiti
+255 777 878 047 – Zanzibar